EAST AFRICANA COLLECTION

MADA: MWAMKO WA WANAWAKE KATIKA TAMTHILIA NNE ZA PENINA MUHANDO

NA: HEZRON MAGOMA NYAMBERI

University of NAIROBI Library
0370573 8

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya "MASTER of ARTS" M. A. katika chuo kikuu cha Nairobi.

1997

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

UNGAMO:

" Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote".

HEZRON MAGOMA NYAMBERI
( Mtahiniwa)

" Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya chuo kikuu".

BW.ZACHARY MUMBO MOSOTI

BW.MWENDA MBATIA

## UNGAMO:

"Tasnifu hii ni kazi yangu

Mwenyewe na haijatolewa kwa

Mahitaji ya shahada katika

Chuo kikuu kingine chochote".

---

HEZRON MAGOMA NYAMBERI

( Mtahiniwa )

---

"Tasnifu hii imetolewa

kutahiniwa kwa idhini yetu

kama wasimamizi wa kazi

hii ya chuo kikuu"

---

BW. MWENDA MBATIA

# YALIYOMO

SHUKRANI

MUHTASARI

SURA YA KWANZA

| | | |
|---|---|---|
| 1:0 | UTANGULIZI .................................. | 1 |
| 1:1 | Tatizo La Utafiti .................................. | |
| 1:2 | Sababu Za Kuchagua mada .................................. | 2 |
| 1:3 | Madhumuni ya Tasnifu .................................. | 3 |
| 1:4 | Upeo Na Mipaka .................................. | 3 |
| 1:5 | Haipothesia .................................. | 4 |
| 1:6 | Msingi wa Nadharia .................................. | 4 |
| 1:6:1 | Ufeministi huru .................................. | 6 |
| 1:6:2 | Ufeministi wa kijamii .................................. | 7 |
| 1:6:3 | Ufeministi wa Kimarks .................................. | 10 |
| 1:6:4 | Ufeministi weusi .................................. | 11 |
| 1:6:5 | Ufeministi unaopinga utawala .......................... | 11 |
| 1:6:6 | Ufeministi asilia .................................. | 12 |
| 1:7 | Yalioandikwa Kuhusu Somo hili .......................... | 14 |
| 1:8 | Njia za Utafiti .................................. | 17 |
| | Tanbihi .................................. | 17 |

## SURA YA PILI

| | | |
|---|---|---|
| 2:0 | Hatia | 19 |
| 2:1 | Utangulizi | 19 |
| 2:2:1 | Itikadi na utamaduni | 19 |
| 2:2:2 | Taasubi ya Kiume | 21 |
| 2:3 | Mwanamke Kiuchumi | 23 |
| 2:4 | Mwanamke Kisiasa | 25 |
| | Tanbihi | 28 |


## SURA YA TATU

| | | |
|---|---|---|
| 3:0 | Heshima yangu | 30 |
| 3:1 | Utamaduni, Itikadi na Mila | 30 |
| 3:1:2 | Ndoa na Mapenzi | 33 |
| 3:2:2 | Taasubi ya Kiume | 35 |
| 3:3 | Mwanamke Kisiasa | 38 |
| | Tanbihi | 39 |

## SURA YA NNE

4:0 Nguzo Mama ................................. 40

4:1 Utangulizi ................................. 40

4:2 Utamaduni ................................. 40

4:2:1 Mapenzi na Ndoa ................................. 41

4:3 Mwanamke Kiuchumi ................................. 44

4:4 Mwanamke Kisiasa ................................. 49

Tanbihi ................................. 54

## SURA YA TANO

5:0 Lina Ubani ................................. 55

5:1 Utangulizi ................................. 55

5:2 Mwanamke Kiutamaduni ................................. 55

5:3 Mwanamke Kiuchumi ................................. 57

5:4 Mwanamke Kisiasa ................................. 60

5:5 Mwanamke Kielimu ................................. 63

Tanbihi ................................. 65

SURA YA SITA

Hitimisho .................................... 66

Bibliografia .................................... 70

TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia wazazi wangu Wilson Nyamberi na Hellen Bisieri kwa juhudi zao za kunielimisha.

# SHUKRANI

Watu wengi sana wamenisaidia kwa njia moja ama nyingine katika kuifanikisha kazi hii. Hapa nitawataja wachache tu. Kwanza nawashukuru wasimamizi wa kazi hii, Bw. Zachary Mumbo Mosoti na Bw. Mwenda Mbatiah ambao masahihisho yao yameniongoza na kunisaidia katika kuipa kazi yenyewe umbo lake la sasa.

Shurkrani nazitoa kwa mwalimu wangu wote. Dr. Kinene wa Mutiso, Dr. Kithaka wa Mberia, Bw. Gichobi Mungania, na Lisanza Mwaka Michira, kwa kunisaidia kwa maoni yao.

Sitawasahau waliochangia kifedha na mahitaji mengine kama ndugu zangu Obang'i, Elijah Nchoga, Nyabassa, Robert Nykeruma, Sarah Nyasaka na wengine. Kadhalika namshuluru mke wangu Elizabeth Nyachama kwa uvumilivu na upweke aliokuwa nao nilipokuwa nikidurusu na kutafiti.

Kwa hakika nimenufaika na maoni ya wanafunzi wenzangu tulipokuwa katika mihadhara mbali mbali kama:- Omondi, olali, Osiemo, Kilelu, Kariuki Ann, Jane, Mbugua na Mutie. Mashauri yao yalinifaidi si hapa. Wao wamenisaidia na kunitia moyo sio kwa maoni nafikira muthmini tu, lakini pia kwa kuniazima majarida na vitabu mbali mbali.

Bi Margaret na Evelyne ambao wamenisaidia si hapa katika kupiga taipu kazi hii. Kwao pia natoa shukrani nyingi.

Ninaamini kuwa kazi kama hii ni zao la juhudi za pamaoja za watu wengi kwa hivyo nawashurkuru sana watu wote wengine ambao walionisaidia na sikutaja majina yao.

**H. M. N.**

# MUHTASARI

Tasnifu hii ni uhakiki wa maudhui ya Mwamko wa wanawake katika Tamthilia Nne za Penina Muhando nazo ni Hatia. Heshima Yangu Nguzo Mama; na Lina Ubani.

Mwongozo wetu katika tasnifu hii ni nadharia ya ufeministi inayorejelea uwakilishaji wa haki za wanawawake kufuatana na imani ya usawa wa kijinsia. Inalenga kupigania kukomeshwa kwa udhalimu wa mwanamke kwa njia yoyote ile. Tumeigawanya kazi hii katika sura sita.

Sura ya kwanza ina somo la utafiti, madhumuni ya tasnifu, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka ya Tasnifu. Aidha tunazungumzia yaliyoandikwa kuhusu mada hii nadharia na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tatu, nne na tano, tumejadili matatizo yanayo wa kumba wanawake katika hali mbali na juhudi zao za kujikomboa na mwisho katika sura ya sita tumehitimisha kazi yetu kwa kuchunguza swala la mwamko wa wanawake kama unavyojitokeza katika maadishi tuliyoyataja.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1:1 TATIZO LA UTAFITI

Jinsi wanawake wanavyowasilishwa katika fasihi ya kiswahili ni swala linalohitaji mtaala kwa vile taswira inayojitokeza kuwahusu ni dhaifu na isiyoonyesha usawa wowote kati yao na wanaume.

Utafiti huu ni uhakiki wa kimaudhui na hususan utajishughulisha katika kuanganzia maovu wanayotendewa wanawake na juhudi zao za kujikomboa kutokana na udhalimu, ugandamizwaji na unyanyasaji wanaotendewa.

Tumelitumia neno "Mwamko" kumaanisha juhudi za kupigania uhuru wao kutokana na udhalimu wa kijamii kisiasa, na kiuchumi. Pia linaweza kuleta dhana ya kuzingatia hadhi ya mwanadamu na katika muktadha huu ni hadhi ya mwanamke.

katika mahojiano ya Adeola (1980:82)1 na Muhando, tunadokezewa maoni yake kuhusiana na swala la ukombozi wa wanawake. Anasema kwamba swala la mwanamke haliwezi kutengwa na maswala mengine ya kijamii. anaamini kwamba ukombozi wa wanawake ni lazima uwe sehemu moja ya ukombozi wa jamii ujumla.

Kwa vile kila tatizo linaloikumba jamii humwathiri mwanamke, muhando anaona kwamba atajishughulisha na maswala yanayomwathiri mwanamke kwa vile asipofanya hivyo wanaume hawatajishughulisha nayo.

Ingawa anadhihirisha hali ya uhafidhina na kutobadilika kwa nafasi ya mwanamke katika jamii, Muhando ameonyesha kuwa mwanamke amedunishwa na kutostawishwa kwa sababu za kijamii. Kazi tutakazozihakiki ni Hatia (1972) Heshima yangu (1974) Nguzo Mama (1982) na Lina Ubani (1984)

## 1:2 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

(i) Sababu ya kwanza iliyotufanya tuwe na hamu ya kushughulikia maudhui ya mwamko wa wanawake ni ule umuhimu wa maudhui yenyewe katika jamii zetu. Swala la mwanamke limeshughulikiwa katika vipengele mbali mbali.

Mkutano wa wanawake huko Beijing (1995)2 ulisisitiza kuwepo kwa usawa na utambuzi wa haki na uhuru wa wanawake kama njia moja ya kuwapatia nguvu. Kutokana na sababu hizi tumeshawishika kwamba tasnifu hii itakuwa ni mchango katika aneo pana la fasihi ya kiswahili.

(ii) Utafiti huu utatusaidia kuzifahamu kazi za Muhando na hatimaye kuweza kuelwa ipasavyo na kupambanua rai kuhusiana na swala la uana katika muktadha wa kiafrika.

(iii) Sababu nyingine ni kwamba mwanamke ameanza kuangaliwa upya. Wasanii nao akiwemo Muhando wanazidi kwangalia jinsi mwanamke alivyo sawiriwa katika fasihi na nafasi aliyopewa katika fasihi na maisha kwa ujumla.

## 1:3 MADHUMUNI YA TASNIFU

Tuta chunguza dhana ya mwamko na hatimaye ukombozi wa wanawake katika tamthilia nne za Penina Muhando. Pia tuta chunguza na kubainisha juhudi zina zofanywa na wanawake ili kujiinua na kujikomboa kutokana na halli zao dhaifu katika mazingira ya jamii walipochorwa. Mwisho tutatathmini faisafa ya mwandishi huyu kuhusiana na maisha ya wanawake.

## 1:4 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu ni wa kifasihi na tutashughulikia elementi ya maudhui katika tamthilia nne za Penina Muhando ambazo ni Hatia (1972) Heshima yangu (1974) Nguzo Mama (1982) na Lina Ubani (1984). Tutajadili kwa undani matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii

(ii) Utafiti huu utatusaidia kuzifahamu kazi za Muhando na hatimaye kuweza kuelwa ipasavyo na kupambanua rai kuhusiana na swala la uana katika muktadha wa kiafrika.

(iii) Sababu nyingine ni kwamba mwanamke ameanza kuangaliwa upya. Wasanii nao akiwemo Muhando wanazidi kwangalia jinsi mwanamke alivyo sawiriwa katika fasihi na nafasi aliyopewa katika fasihi na maisha kwa ujumla.

## 1:3 MADHUMUNI YA TASNIFU

Tuta chunguza dhana ya mwamko na hatimaye ukombozi wa wanawake katika tamthilia nne za Penina Muhando. Pia tuta chunguza na kubainisha juhudi zina zofanywa na wanawake ili kujiinua na kujikomboa kutokana na halli zao dhaifu katika mazingira ya jamii walipochorwa. Mwisho tutatathmini faisafa ya mwandishi huyu kuhusiana na maisha ya wanawake.

## 1:4 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu ni wa kifasihi na tutashughulikia elementi ya maudhui katika tamthilia nne za Penina Muhando ambazo ni Hatia (1972) Heshima yangu (1974) Nguzo Mama (1982) na Lina Ubani (1984). Tutajadili kwa undani matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii

anayoishughulikia. Zaidi ya hayo tutadadisi jinsi anavyoendeleza maswala ya wanawake najitihada zao za kujikomboa.

Kwa kiwango kikubwa utafiti huu utajikita katika tamthilia nne tulizozichagua na inapolazimu tutatoa maoni kutoka tamthilia zake, zingine na maandishi mengine yanayochangia mada yetu.

## 1:5 HAIPOTHESIA

Muhando anatambua matatizo yanayowakumba wanawake na anapendekeza njia za kuyashughulikia.

## 1:6 MSINGI WA NADHARIA

Hatutajishughulisha na aina mbali mbali za nadharia katika tasnifu yetu. Tutaangalia kwa muhtasari tu aina ya nadharia ambayo tunadhani itatufaa katika utafiti wetu. Nadharia ambayo tumeichagua ili kuongoza tasnifu hii ni ile ya kifeministi. Ufeministi ni dhana inayotokana na neno la kilatini "Femina" lenye maana ya Mwanamke. Dhana hii inarejelea uwakilishaji wa haki za wanawake kufuatana na kuambatana na imani ya usawa wa kijinsia. Huu ni mwamko wa wanawake unaolenga kupigania kukomeshwa kwa udhalimu dhidi ya mwanamke kwa njia yoyote ile.

Bunch (1981)3 anaonelea kwamba nadharia ya kifeministi inajishughulisha na mabadiliko yanayolenga kuunda upya jamii kuhusu nafasi ya mwanamke. Hivyo nadharia hii hutumiwa kwa upana wake kurejelea mwelekeo wa yeyote anayetambua kung'amua na kujitahidi kukomesha ugandamizwaji wa wanawake.

Kulingana na maoni ya Engels (1884)4 mabadiliko yaliyotokea yenye ustaarabu ndiyo yaliyosababisha udhalimu wa wanawake. Jamii asilia ili kuwa na utathimini sawa wa kazi za wanaume na wanawake. Baadaye mabadiliko yenye ustaarabu yalianzisha urithi upande wa baba, Haya yalitokana na hali ambapo kazi za wanawake za uwindaji na ufugaji zilipoanza kuleta faida zaidi kuliko kazi za nyumbani. Ongezeko la mali upande wa baba ulizusha kuwepo kwa mali ya kibinafsi na hivyo wanawake wakaanza kuwategemea wanaume kiuchumi.

Kutokana na hali kama hii wananadharia ya kifeministi wanajitahidi kufichua nyanja za udhalimu pamoja na kuibua mikabala na mikakati ya kufikia ukombozi wa wanawake.

Msingi wa nadharia hii ni katika Virginia Wolf (1928) A Room of One's Own iliyoasisi nadharia hii. Mary Wolstone Craft (1962) A Vindication of The Rights of Women, alisisitiza umuhimu wa kuboresha elimu kwa wanawake. Amendelea kusema kwamba umuhimu

wa nadharia hii ni kule kudadisi mifumo ya jamii nyingi inayoelekea kumtukuza Mwanamume na kumtweza mwanamke huzitazama asasi mbali mbali zinazokuza na kuendeleza udhalilishaji wa mwanamke. Wananadharia ya ufeministi wanaonelea kuwa mwanamke hana budi kuzipinga asasi kama hizo. Hivyo dhamira ya wanaharakati wa nadharia ya ufeministi ni kuwaunganisha wanawake dhidi ya wanaume ili kujikomboa kutokana na silisila za wanaume.

Tuna matawi kadhaa ya nadharia ya kifeministi, hayo tutayaelezea kwa juu juu lakini kwa madhumuni ya tasnifu hii tutatumia tawi la ufeministi asilia.

## UFEMINISTI HURU

Tawi la ufeministi huru ndilo tawi linalojulikana zaidi na ndilo la kwanza kuibuka. Tawi hili lilikuwepo katika enzi ya ukombozi wa karne ya kumi na nane. Msingi imani wa tawi hili ni kwamba wanadamu wote wanazo haki za kiasili ambazo hasipaswi kubatilishwa.

Wolstonecraft (1962) ndiye mwanafalsafa wa kwanza kuibuka na tawi hili la ufeministi huru. Madai yake ni kuwa usawa na haki na nafasi zinapaswa kusambazwa kwa wanawake katika nyanja zote za maisha. Alipigania haki sawa kupitia mabadiliko ya kisheria na kijamii.

Wanadharia wa tawi hili wanatoa madai kuwa wanawake wamebaguliwa kwa sababu Wanachukuliwa kuwa ubinadamu wao huja katika nafasi ya pili na wanaume huchukuliwa kulingana na thamani yao si kwa majibu wa utuna. Tawi hili limeibuka kwenye misisngi kuwa mwanamke hubaguliwa kwa sababu ya uwana na hivyo hujishughulisha na usawa na haki kazini siasa elimu na hali ya jumla ya kimaisha.

Richards (1962:14)

Upungufu wa tawi hili ni ule wa kutochunguza chanzo cha udhalimu unaofanyiwa Wanawake. Tawi hili linaonekana kuwa la kimadili zaidi na hukosa zile cheche za kimapinduzi katika jamii bila kuzingatia mifumo iliyopo na inayotawaliwa na kasumba iliyosakini ya kiume.

## UFEMINISTI WA KIJAMII

Ufeministi wa kijamii nao unalenga kuvunjilia mbali matabaka na pia jinsia. Hudhamiria kuleta mapinduzi katika kaida za kijamii zina zotawaliwa na uume ukapitalisti.

Wafuasi wa nadharia hii kama Neil na Naomi Black wana lengole kukomesha dhuluma za aina zote na kuunda jamii isiyotambua misisngi ya uwana. Imani yao ni kuwa ubinafsi wa binadamu una uhusiano na siasa za kijamii.

Nadharia hii inaangalia maswala yote yanayohusu ukombozi wa wanawake kihistoria. Wafuasi wake huunga mkono kuwepo kwa utenganisho na uhuru wa kuwepo na chama cha ukombozi wa wanawake. Wanashikilia kuwa wanaume mbali na mfumo kwa jumla wanaonekana kama adui.

Banks (1981:8)5 anasema kwamba ingawa watu. Wengi wanamini kuwa ufeministi wa kijamii umepewa nguzo na umarks, nadharia hii ilijibuka katika enzi za zamani inatokana na chama cha saint Simononian huko Ufaransa. Wamachama wa kundi hili walipinga utamaduni wa nyumbani na wakapendekeza mfumo wa kijamii ambapo malezi ya watoto yatakuwa jukumu la jamii nzima.

Hata hivyo nadharia hii imechangiwa pakubwa na umarks ndipo Jaggar (1983:125)6 anadai kuwa:

> Uhakiki wa kijamii wa
> Kike ni wa kimarks kwani
> Unatumia dhana ya uyakinifu wa kihistoria.

Ili kuelewa uhusiano kati ya wanaume na wanawake, nadharia hii ina mgawo wa kiuana wa kazi katika jamii. Wanaamini kuwa tofauti kati ya waume na wanawake ni za kimaumbile na kisaikolojia. Saikolojia ya

uume na uke hutokana na jinsi watoto wadogo wanavyolelewa katika jamii fikra na mawazo yao huundwa kiuana na jamii wanamokulia. Katika kuelezea saikolojia ya binadamu wananadhania hii wanasema:-

(i) Maisha yetu ya "ndani" miili na hulka zetu huundwa na hali zetu za kiunana.

(ii) Muundo huu wa kiuana sio wa kimaumbile bali umesababishwa na jamii

(iii) Jamii nayo hurithi muundo huo kutokana na mfumo wa kihistoria wa uzalishaji mali wa kibepari kikapitalisti na kiume

(iv) Muundo wa kiuana wa maisha yetu ya ndani hutokea tukiwa bado wachanga na huendelewa maishani kupitia asasi tofauti tofauti za kijamii.

(v) Hali hii ndiyo hasa inayoendeleza na kukuza tawa la kiume katika jamii Waitifaki wa nadharia hii wanakubaliana kuwa kuna umuhimu wa kuweza kutambua na kutukuza kazi za uzazi, malezi nakwa jumla kazi zote za kinyumbani zina zofanywa na wanawake.

Kwa ujumla ina washutumu wanawake wasioshiriki kwa jinsi wanaovyoshindana ili kuteka hisia za wanaume.

## 1:6:3 UFEMINISTI WA KIMARKS

Ufeministi wa kimarks unachukulia kuwa ugandamizwaji wa mwanamke ni aina moja ya dhuluma zilizosambaa katika dunia duara. Ruthuen (1984:28)7 anatuelezea kuwa mtazamo wa umarks huashiria ubepari, nyenzo za uzalishaji mali na umilikaji wa mali kama kitovu na hivyo chanzo cha dhuluma zote.

Marx alionelea kuwa dhuluma dhidi ya mwanamke zitaisha pale ambapo dhuluma dhidi ya wanyonge wote zitakuwa zimeondoshwa baada ya mfumo wa kibepari kuangamizwa. Einstein (1975:5) anaeleza kwamba ukandamizwaji wa wanawake na wanaume ulikuwepo hata kabla ya majilio ya mfumo wa kibepari ingawa mfumo huu baadaye uliuendeleza. Dhuluma ya mwanamke ilianza wakati mwanaume alipomtengea kazi si- zisoifaida. Hali hii ilimfanya mwanamke amtegemee mwanamume ~~la~~ hivyo mwanamume akapata nafasi ya kumkandamiza. Engels (1944)

Ajenda muhimu ya waitifaki wa nadharia hii ni kupinga kaida za urithi na umilikaji mali zinazombagua mwanamke. Wapinzani wanaiona nadharia hii kuwa haistahili kutalii ugandamizwaji wa wanawake na

wanaume na mifumo ya kijamii kwa unyeti unaohitajika. Wanasema kuwa nadharia hii huyaangaalia matatizo ya mwanamke katika, mkabala wa matatizo yanaoyoikabili jamii duara, wakidai kuwa nafasi ya mwanamke katika jamii hahitaji kuboreshwa nakuimarishwa kwa Mapinduzi ya dharura.

## 1:6:4 UFEMINISTI WEUSI

Ufeministi weusi uliibuka nchini Marekani na wanawake weusi. Ingawa kulikuwa na makundi mengi yaliyoshughulika ukombozi wa mwanamke wengi wasio weupewalionelea kuwa hawakuwasilishwa vya kutosha katika makundi hayo.

Giddings (1984) anasema kwamba wanawake weusi walibaguliwa kwa sababu walikuwa weusi na pia kama wanawake. Walijiona wame kabiliwa na ubaguzi wa kiuana na rangi. Hata hivyo waliona kuwa ubaguzi wa rangi ulichukua nafasi kubwa kuliko ule wa kinana. Hata hivyo baadaye wanadharia hii walianza kupinga ukandamizwaji wa aina yoyote ile.

## 1:6:5 UFEMINISTI UNAOPINGA UTAWALA

Ufeministi unaopinga utawala ulitambuliwa mwanzo wa miaka ya sabini. Mizizi yake ni neno la kigiriki "Anarcho's" linalomaonisha bila mtawala.

Wafuasi wake wanaamini kuwa ubaguzi wa kiuana una uhusiano na maumbo yote ya udhalimu na mahusiano ya kiutawala. Wanapinga kuwepo kwa tawala za aina zozote, madaraja ya uwezo na mahusiano ya kiutawala.

Wanaamini kuwa tawala zote huwa fisadi na zinapaswa kuvunjiliwa mbali na mahali pake pakachukuliwe na mahusiano ya misingi ya uelewano na ushirikiano wa kihiari.

## 1:6:6 UFEMINISTI ASILIA

Kwa mujibu wa Utafiti huu tutatumia nadharia ya ufeministi asilia kwa sababu nadharia hizi zingine hazikuwa na dhana Maalum za kuelezea utawala wa kiume waliona kwamba utawala wa kiume ni wa kawaida na unaotarajiwa ilhali tawi hili lilichukulia kwamba utawala wa upande wa kuumeni ndio unafaa kuelezea uundaji na huendelezaji wa utawala wa kiume kijamii kiitikadi, kisiasa na kiuchumi.

Tawi hili liliibuka miaka ya sitini na waliochangia katika kulikuza na kuliendeleza ni kama Firestone, Hole na Ravine (1971) Freeman (1978) wafuasi hawa wana imani kuwa kubaguliwa kwa mwanamke ndio mzizi wa maonevu yote.

Teneti muhimu zina zoifanya nadharia hii kuwa maarufu ni kama zifuatazo. Kwanza ni ile hali ya kupinga kisiasa nafasi duni ya mwanamke. Huanza kwa swala la kutokuwepo kwa usawa kati ya wana na hutafuta kuunda upya jamii kwa kuamini kuwa mabadiliko ya juujuu hayatabadili miundo ya ndani ya kijamii. Kwao mwanamume anaonekana kama adui anayefaidi kutokana na magandamizo ya mwanamke na kwamba njia pekee ya kukomesha hali hii ni kutengana naye kabisa na kuishi katika jamii yao.

Vile vile walipinga mfumo wa urithi wa kuumeni wakidai kuwa urithi haupaswi kuegemezwa katika uana kama kwamba wanawake si wanadamu. Walikusudia kuwaunganisha wanawake ili wajipiganie kama kundi moja wakilenga kujikomboa kwa kuzua taswira chukivu kwa mwanamume ambaye alipaswa kuchukuliwa kama adui mkubwa.

Walitaka kujitenga kabisa katika maisha na kuanzisha utamaduni wa mwanamke, kuwa na mataifa yao, vyama vyao na hata biashara zao. Kwa kiwango kikubwa walipinga asasi zinazohalalisha udhalimu dhidi ya mwanamke hasa ndoa uzazi na maingiliano ya kimwili kati ya mwanamke na. Mwanamume ufeministi asilia unawahimiza wanawake washerekee hali zao za kike ambazo wanadai kuwa ni bora kuliko za kiume.

Aidha nadharia hii inatetea jamii ambapo hakutakuwa na hali ya kugandamizwa na kutawaliwa kwa nguvu. Inatilia maanani uhuru na usawa unaokubaliwa na wanajamii na kuishi kwa kuadhimisha na kuheshimiana. Kwa ujumla nadharia hii itatusaidia katika utafiti huu kwa inajishugulisha na juhudi za kumkomboa mwanamke ambalo ndilo lengo la utafiti huu.

## 1:7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Swala linalohusu wanawake ni pana sana na kuna maandishi si haba ambayo yameandikwa kuhusu swala hili. Hata hivyo tutatoa maoni machache ambayo yatatusaidia kufanua na kuendeleza tatizo la utafiti wetu.

Kazi yetu inatofautiana na kazi nyingine kwa sababu sisi tumejikita katika nyanja maalum yaani "mwamko wa wanawake katika tamthilia nne za Penina Muhando."

Dhahabu (1994) Anachunguza Uumbaji na Uendelezaji wa wahusika katika tamthilia nne za Penina Muhando. Tamthilia hizo ni <u>Tambueni Haki Zetu</u> (1972) <u>Talaka si Mke Wangu</u> (1976) <u>Nguzo Mama</u> (1982) na <u>Lina Ubani</u> (1984). Kwa maoni yake anachunguza kipengele hiki cha wahusika na kuona jinsi hali zao zinavyoathiri uwasilishaji wa maswala

makuu yanayojadiliwa.

Kazi hii ni muhimu katika uchunguzi wetu kwa sababu tutachunguza wahusika wa kike na kudhihirisha ikiwa wana hisia za kiukombozi dhidi ya dhuluma wanazofanyiwa.

Hata hivyo utafiti wetu ni tofauti kwani utajushughulisha na maswala ya wanawake na hasa maudhui ya mwamko wa wanawake na ilhali Dhahabu anajishughulisha na kipengele cha Fani.

Kiango (1992) ameangalia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Anasema kuwa mwanamke anaonyeshwa kama mtu ambaye hana usawa na mwanamume na pia kama kitega uchumi, mbaya, mzinifu, mtoaji mimba na mtupaji watoto. Anapohakiki tamthilia ya Kilio Cha Haki anasema kuwa inastahili kupewa nafasi ya kipekee kwa sababu mkabala wa Mazrui ni tofauti na waandishi wengine.

Kazi hii itatusaidia kuendeleza maudhui ya ukombozi. Hata hivyo Kiango hakuzama katika misingi ya hali hizi alizozidhihirisha kama tutakavyofanya katika utafiti huu.

Lugano (1989) akishughulikia wahusika wa kike katika Riwaya nne za kezilahabi, ameelezea jinsi kezilahabi alivyowasawirii na jinsi walivyoathiriwa na mifumo mbali mbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kazi hii itatufaidi kwani tutachunguza namna vipengele vya kiuchumi kisiasa nakijamii vinavyochangia katika kumtweza mwanamke jinsi watakavyopigana dhidi ya hali hizo za kijamii. Utafiti huu unashughulikia riwaya hivyo tofauti na wetu unaohakiki tamthilia.

Mbughuni (1982) anashugulikia taswira ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili hasa riwaya zilizoandikwa nchini Tanzania. Anasema kwamba nafasi ya mwanamke nchinini Tanzania ni ya hali ya chini hata ingawa Chama Cha TANU kina dhamiria kuleta usawa kati ya wana. Anaona kwamba katika Uumbaji wa wahusika wanawake hawajawndelezwa kwa njia yoyote wanajitokeza kama wawakilishi wa maovu.

Kazi hii ina mchango katika uchanganuzi wetu kwa vile inaangalia swala la kudunishwa kwa wanawake ambalo tutalishughulikia, hata hiyo tutapiga hatua katika kuonyesha kuwa hawadhiriki na hali zao duni bali wanajitia katika harakati za kujikomboa.

Mochiwa (1976) Matheru (1975) na (1987) wamechunguza kwa ujumla maudhui ya tamthilia za Penina Muhando. Kazi hizi zimeelezea maudhui kwa ujumla na hivyo tofauti na kazi yetu inayochunguza maudhii ya mwamko wa wanawake katika baadhi ya kazi zake.

Kazi zingine zenye manufaa kwetu ni kama vile Lisa (1986) Banks (1981) Ramazangolu (1989) Mitchel, Juliet and Oakley (1986). Kazi hizi zimeangazia kwa undani nadharia ya ufeministi ambayo ndiyo mwongozo wa tasnifu hii.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu utajikita katika maktaba na utahusu kusoma kazi za Penina Muhando na zile za kifeministi.Tena tutasoma vitabu na makala yanayozingatia swala la wanawake ili kupanua mawazo yetu kuhusu somo hili.

### TANBIHI

1. Adeola J (1980) In Taheir own voices James currey London.

2. United Nations: The Beijing declaration and platform for Action. 4th Beijing China World Conference on Women Beijing China 4-15 September 1995. Pg.2.

3. Bunch (1981)

4. Engels F.(1844) Origin of the Family, Private Property and the State. Charles H. Kevin and Company Cooperative Chicago. uk.74

5. Banks O.(1981) Faces of Feminism. A study of Feminism as a social movement. Basil Blackwell Ltd London. uk. 8

6. Jaggar (1983)

7. Rethuen K.(1984) Feminist Literary Studies. Cambridge University Press,
London uk. 28.

# SURA YA PILI

## HATIA

2:0

2:1 UTANGULIZI

2:2 MWANAMKE KIJAMII

2:2:1 ITIKADI NA UTAMADUNI

Hizi ni baadhi ya taasisi zinazotumika kuwagandamiza wanawake katika jamii. Mara nyingi jukumu la utamaduni ni muhimu katika maendeleo ya jamii hasa tunapolihusisha na nafasi ya mwanamke.

Cheja kama wasichana wengine wa kisasa ameasi utamaduni wa kijadi ndiposa anafanya mapenzi na Juma huku akidhamiria kuwa angeolewa naye. Msimamo wa jamii kongwe ni kuwa mipango maalum ilihitajasika katika mahusiano ya kimapenzi na hatimaye ndoa.

Kwa sababu ya mazingira ya kimji Cheja anaamua kufanya mahusiano ya kimapenzi na kijana mwenzake bila kuwahusisha wazazi. Hali kama hii ina tudhihirishia kuwa itikadi na tamaduni zisizofaa hazitadhumu na hivyo Cheja anaamua kuenda kinyume cha matarajio ya jamii kongwe.

Ingawa matokeo ya mahusiano haya yalisababisha mimba isiyotarajiwa jinsi Cheja anavyokabiliana na tatizo hilo linatuonyesha kwamba mwanamke akipewa nafasi anaweza kujikomboa kutokana na hali yake dhaifu.

Wazee na tamaduni zao hazikumsaidia Cheja. Hali hii inatuonyesha kwamba jamii inabadilika hivyo wanawake wanapaswa kupewa nafasi sawa na masilahi yao kutetewa. Kile kitendo cha Cheja kuamua kujitenga na kuanza kuishi pekee kijafungamana na nadharia ya ufeministi yetu inayosistiza kwamba ikiwa wanawake wanataka kujikomboa ni heri wajitenge na wanaume wanaowanyanyasa na kuwagandamiza. Aidha tamaduni zinazohalisha ugandamizwaji na kutomthamini mwanamke kama mtu mwenye hadhi na heshima katika jamii zinafaa kuvutiliwa mbali.

Matatizo yanayowakumba wanawake yanatokana na kuwategemea wanaume na utiifu kwa utamadunina itikadi. Hivyo wanawake wanahitaji kujibidiisha ili kujitegemea na kuanza kujiendeshea maisha yao binafsi kama alivyo fanya Cheja. Anaamua kuishi pekee na kuendesha maisha yake bila kujihusisha na chuma aliyemdhulumu au baadaye kum-tupilia mbali.

2:2:2 <u>TAASUBI YA KIUME</u>

Kuonewa kwa wanawake na wanaume. Kiburi cha wanaume kujitwaza kwao na kutojali kabisa mambo yanayohusiana na wanawake. Baadhi ya wanaume wanawaona wanawake kama mitambo ya kuzaa au kutosheleza tamaa za miili ya wanaume. Juma kwa mfano anatafuta starehe ndiposa hataki kutiwa lawamani ya kumpatia cheja mimba.

| | |
|---|---|
| JUMA | Mimi nakwambia usiniingize kwenye janga hili. Sina shughuli nalo. Tena nakueleza usije ukalogwa kumwambia mtu kuwa mzigo huu ni wangu. Walahi utajuta ( uk.8 ) |

Kutokana na dondoo hili tunadhihirishiwa hadaa ya wavulana kwa wasichana. Lawama zote zinamwendea msichana anapopata mimba. Juma anamtisha Cheja anapotaka washauriane kuhusiana na mimba aliyompatia. Hataki waongea kuhusu jambo hilo la mimba na utunzaji wa mtoto atakaye zaliwa. Anatumia ujanja na vitisho kumgandamiza Cheja.

Wazo la Juma kumshauri Cheja kurudi nyumbani kwao hakutamsaidia kwani jamii hairuhusu msichana kupata watoto nje ya ndoa.

JUMA Jiendee zako kwa wazazi wako ukajitunze, kama unaogopa kuendelea kukaa kwa mwajiri wako ( uk 9 )

Hapa mwanamume anaonekana kuwa mwenye hadhi kuliko mwanamke. Hali ya mwanamke ni ya kudhalilishwa ilhali ya mwanaume imkwezwa mwanamke anadhihirika kama kiumbe asiye na hisia na kuwepo kwake ni kwa ajili ya kutimizia shauku za kimwili za mwanamume.

Muhando anapoendekeza kuwa ili kujitaunzua kutokana na hali kama hizi. Anaona kuwa vijana wanahitaji mafunzo na elimu maalum juu ya ujana, mapenzi na maisha kwa ujumla. Cheja anaamua kuishi pekee kinyume na matarajio yake.

Hata hivyo kulingana na nadhariza ya ufeministi asilia kujitenga kwa wanawake kutokana na wanaume ndio via inayofua ya kumkomboa mwanamke. Waitifaki wa nadharia hi wanasisitiza kufutilia mbali kwa ndoa. Kwao ndoa ni kikwazo an kizuizi kikubwa katika kufanikisha maendeleo ya mwanamke kwani inamfunga kwa majukumu na nifumo ambayo wanaiona kuwa ni ya kudunisha na kuvunjilia heshima kwa jamii ya mwanawake.

## 2:3 MWANAMKE KIUCHUMI

Mwanamke kama anvyojitokeza katika jamii hii anatokana na mazingira yaliyojaa umaskini. Aidha umasikini huu unatokana na unyonge wa mwanamke kiuchumi kwa sababu ya kutoshirikishwa sawa kiuchumi hivyo kunyimwa uwezo wa kujitegemea.

Kazi nyingi zina zofanywa na wanawake kama zinavyodhihirika katika tamthilia hii ni zile za nyumbani ambazo hazidhamininiwi wala hazina faida ya kiuchumi. Engels (1844) anasema kuwa ta fauti kati ya mwanaume na mwanamke zimetokana na ugawanyaji wa kazi tangu enzi za giza na kuendelezwa hadi sasa.

Wanawake katika tumthilia hii wanajitokeza wakipepeta mahindi. Maoni ya kina bibi hawa ni kwamba wanawake wametegewa kazi kama hizi. Hivyo licha ya Bi Chowe kulalamika kuwa ni kwa sababu ya umasikini ndipo Cheja akaenda Dar-es-Salaam kufanya kazi Mwanamke I na II wanaona kuwa hata angeolewa jukumu lake linge kuwa lile la kufanya kazi bila usaidizi.

MWANAMKE I: Thubutu! Angekuwa ameshaolewa anawafanyia kazi wakwe zake na wewe ungebaki hapa hapa (uk. 10)

Hali hii inatudhihirishia kuwa endapo mwanamke anaolewa huwa anafanya kazi ya kuendeleza jamii ya mumewe. Hivyo anakuwa kama chombo cha kuzalisha mali.

Aidha msichana katika jamii nyingi za kiafrika anadhihirika kama kitega uchumi au chombo cha kuleta faida. Tunadhihirishia kwamba baada ya Cheja kuolewa ndipo Mkami angepata mahari ya kuolea. Naye Mzee Chowa analalamika kwa kukosa hadhi mbele ya wazazi wenzake na mali aliyoitumainia ikiwa cheja angeolewa kufuatana na misingi ya kijamii.

Wote hawa walidhaminia kupata mali baada ya cheja kuolewa na ndiposa Sembuli anapofikishwa mbele ya wazee, wanamlazimisha kutoa mahari hata kabla ya kufahamu ukweli wa jambo wanalomstakia. Mkami anapenekeza mahari ambayo angetarajia.

Mkami: Ng'ombe saba mbuzi tisa na kuku watatu. (uk 18)

Doundoo hili inatuony esha jinsi ambavyo mwanamke amethiriwa na harakati za kiuchumi. Wazazi wengi huwaona binti zao kama njia moja ya Kujitajirisha bila kujali athari zake. Kwa kutudhihirishia hayo Muhando anajitokeza kupinga mahari yanaoombwa na wazazi. Vile vile anatuonyesha kuwa swala la mahari halipaswi kuwekwa mbele. Kule kukosa fidia ambayo Mkami na Mzee Chowa waliyotarajia ni thibitisho wazi kuwa mahari hayana nafasi yoyote katika jamii. Hivyo

katika kumkomboa mwanamke ni lazima swala la mahari lichunguzwe upya namwanamke kupewa hadhi anayostahili. Hali kama hii inajitokeza katika tamthilia ya **Uiasi 2.** Riziki anatoroka na kuolewa na John na hivyo kumfanya Mzee Nyamawi kukosa mahari aliyo tarajia. Vile vile Lanina katika **kilio cha Haki 3** anaoneka kuwa muasi kwa sababu anapigania haki za wafanya kazi. Lakini tunaona kuwa juhudi zake zinaleta mzinduko katika hisia za wafanyakazi kuweza kupigania haki zao za kazi. Ingawa alinyimwa haki yake ya kiuchumi na kudhulumiwa na jamii ambazo zinatawaliwa na wanaume anaamua kupigana hadi mwisho. Ndipo anasema kuwa atarudi hata ingawa ni kifuoni.

## 2:4 MWANAMKE KISIASA

Jamii nyingi za kiafrika hazimpi mwanamke nafasi ya kufanya maamuzi kuhusuru maisha yake akiwa bado hajaolewa au anapoolewa.
Iwapo ni msichana baba ndiye ataamua kwa niaba yake. Jambo kama lilo Linatuonyesha wazi kuwa wanawake hawashirikishwi katika kuleta mabadiliko ya sheria za jamii zina zomgandamiza na kumnyima haki na uhuru wake.

Katika tamthilia hii Muhando anatuonyesha jinsi Wazee wanavyoshikilia mila na desturi hivyo hawakubali mwanamke kuja kutoa ushahidi mbele yao.

SEMBULI: Yuko wapi Cheja mwenyewe mwiteni aje aeleze kama ni mimi nimefanya hivyo.

MZEE I: Wazee sasa mnataka kujidharau wenyewe pamoja na jadi yetu. Mna maana kuwa sisi Wazee wote na mvi zetu tumeshindwa na jambo hili hata tumwite mwanamke tena mischana mdogo. (uk 21)

Kutokana na dondoo hili tunawza kusema kwamba mwanamke anadhihirika kama mtu ambaye hawezi kutoa uamuzi wowote mbele ya wazee.

Aristotle (1988)4 anasema kwamba maishani wanawake huwa chini ya utawala wa wanaume. Utotoni wanajinyenyekea kwa baba zao na wanapoolewa hujinyenyekea kwa wanaume wao, hali hii ndiyo inayozingatiwa na jamii za kiafrika. Hivyo inakuwa vigumu kwa msichana kama Cheja kujitokeza mbele ya hadhara ili kutoa kauli zake.

Mwanamke hashirikishwi katika kutafuta njia za kulifatua tatizo la Cheja. Bi Chowe hakupewa nafasi yoyote ya kuchangia katika kutatua tatizo la mtoto wake wala Cheja mwenyewe. Hali hii inadhihirisha kwamba hakuna usawa katika jamii.

Kulingana na nadharia ya ufaminishi asilia mifumo yote ya kijamii inayo tumiwa kungandamiza mwanamke inapaswa kubadilishwa na kuunda njia mpya za kisiasa ili kupata miundo mipya Ramazanoglu (1989.45)5. Mchezoni mwanaume anaonekana kama mtu mwenye kauli kali, nzito na isiyohitaji maja diliano. Hili ni jambo lisilofaa ikiwa tunajali masilahi ya wenzetu.

Mugambi (1983)6 anasema kwamba mwanamke amebanwa na kupewa sifa za mnyonge asiye na nguvu wala uwezo mbele ya mwanaume lakini angali anajaribu kupinga lali hiiduni. Hivyo baada ya wazee kushindwa kupata suluhisho mwafaka, Cheja anafanya uamuzi wa kibinafsi. Anaamua kujiunga na watu wengine kaatika kijiji cha Majogoo. Hali hi ya kuishi pekee nakufanya muaamuzi yake ni dhihirisho wazi kuwa ili kujikomboa mwanamke anastahili kujitambua kama mtu ambaye ana haki ya kujiendeleza. Anarudi kijijini na kuanza maisha mapya ya kujitegemea.

Tatu katika **Wakati Ukuta 7** anaamua kuolewa na swai licha ya pingamizi ya wazazi wake hasa Ma Tatu. Linalohitajika ni utetezi wa wanawake ili kujikomboa kama alivyofanya Cheja.

TANBIHI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Engels F. | (1844) | The Origin of the Family Private Property and the State, Charter H. Kerr and company Cooperative chicago |
| 2. | Kitsao J. | (1980) | Uasi oxford university press Nairobi |
| 3. | Mazmi A. | (1981) | Kilio Cha Haki, Longman Nairobi |
| 4. | Aristotle | (1988) | The Politics cambridge university Press London UK 7 |
| 5. | Ramazanoglu C. | (1989) | Feminism and The contradictions or Oppression routledge London. UK 12 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Mugambi K. | (1983) | "Kilio Cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohammed." Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi. |
| 7. | Hussein E. | 1970) | Michezo Ya Kuigiza East African Publishing House Nairobi |

## SURA YA TATU

## HESHIMA YANGU

**3.0**

3.1 UTAMADUNI, ITIKADI NA MILA

Dhana ya utamaduni hutumika kurejelea maisha ya watu, jinsi wanavyiona na kutenda mambo yanayowatambulisha kama kikundi maalum. Huwa kama kioo kinachodhihirisha amali, na taratibu za jamii husika. Pia utamaduni umechukua nafasi kubwa na muhimu ili kutudhihirishia nafasi ya mwanamke katika jamii. Aidha mila,itikadi na wanawake katika hali mbaya.

Katika tamthillia hii Mamake salum ananyanyaswa kwa vile jamii na utamaduni kwa ujumla unakubali kuwa kosa la kupata mimba isiyotarajiwa ni la mwanamke pia analaumiwa kwa kitendo cha kufanya mapenzi ovyo.

Ni jambo lililo wazi kuwa mwanamume na mwanamke wanashirikiana katika kitendo cha ngono lakini shituma zote humwendea mwanamke. Hivyo Mama salum hawezi kupinga kwani jamii hii inamwekea mwanamke lawama. Hali kama hii inatokana na unyonge na umaskini wa mwanamke unaomfanya kutoweza kupinga dhuluma kama hii.

Kulingana na nadharia ya ufeminiti swala la ngono lime shughulikiwa tangu awali. Waitifaki wa nadharia hii wamepinga hali ya kuwafanya wanawake kuwa kama vyombo vya kukinaiza uchu wa mwanaume katika ndoa na nje ya ndoa. Mzee Isa ana mke wake wa halali lakini anaendelea kufanya mapenzi na Mama Salum.

Baada ya Mama Salum kupata mimba Mzee Isa anamfanya kuishi katika hali ya kutofichua siri hii kwa zaidi ya miongo miwili. kinachojitukeza ni kwamba wanawake wanaangaliwa na kuhukumiwa kwa matendo yao bila kufikiria matendo hayo yameletwa na nani.

Aidha ni kutokana na ukosefu wa itikadi murua ya uchambuzi kunakomfanya mwanamke apewe picha isiyo nzuri na potofu. Mama Salum anapopata urazini tunaona kuwa anaanza kupinga hali yake ya awali. Anaanua kutoboa siri ya miaka kadhaa. Anamweleza Salum ukweli na uzazi wake na hivyo kuvunjilia mbali uhusiano uliokuwepo kati ya Salum na Rukia. wao ni ndugu na kwa desturi na mila za kiafrika watu ambao wana uhusiano na damu hawawezi kuoana.

> MAMA SALUM     Huwezi kumwoa Rukia. baba yako huyu hapa- Mzee Isa (uk 19).

Dondoo hili linatudhihirishia kuwa, ikiwa wanawake wanataka mapinduzi halisi lazima wapigane kwani amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Uamuzi alioufanya Mama salum wa kuelezea uovu wa Mzee Isa unafaa.

Kitendo chake ni dhihirisho wazi kuwa udanganyifu na vitisho vya wanaume havitadumu ikiwa wanawake watajitia katika harakati za kujikomboa na kutetea hadhi na nafasi yao katika jamii inayodhihirisha uganda mi zwaji na unyanyasaji.

Mama Salum aliachiwa jukumu la kumlea mtoto baada ya Isa kuamua kutojishughulisha na ulezi wa mtoto. Sababu ni kwamba hakutaka kuvunjiwa heshima yake. Ingawa hakueleza siri ya kumlea na kumtunza mtoto kwa miaka ishirini na mitano bila msaada wa, Isa baadaye anaamua kuueleza ulimwengu siri hiyo. Hivyo anaonyesha mwamko fulani kuhusiana na dhuluma aliyo fanyiwa miaka kadhaa iliyopita.

3:2:1 <u>NDOA NA MAPENZI</u>

Mapenzi kati ya Salum na Rukia yanadhihirika kuwa ya kweli. Tunaona kuwa hata wamejitayarisha kufunga mbingu za maisha. Licha ya mipango yao tunaona kuwa kuna vikwazo kutoka kwa wazazi.

Vijana wanahitaji kupewa uhuru wa kuchagua mpenzi. Hii ni kutokana na. Mabadiliko tunayoshuhudia katika jamii. Riziki katika **Liasi 1** na siti katika **zabibu chungu 2** wanapinga kutafutiwa wachumba. Riziki na Siti hawakubali kuolewa na wanaume wazee ambao wamechaguliwa na wazee wao. Wote wanatoroka siku ya harusi na kuolewa na vijana wanaowapenda. Kinachojitokeza katika tamthilia hii ni kwamba mwanamke hana uhuru wa kumchagua mpenzi wake. Mzee Isa bado anashikilia zile mila za jadi kuwa ni jukumu lake kama mzazi la kumchagulia mtoto wake mume wa kumwoa.

**MZEE ISA:** Wewe! (kwa nguvu) ngoja nikukute huko nyumbani (amgeukia salum), Na wewe kijana wee, mimi najua watu wa kumwoza binti yangu siyo mtu kama wewe usiye na baba, mjomba wala baba, shangazi.

Kutokana na dundoo hili tunaona kuwa wazazi wanajitokeza kuwa wapinzani wa mahusiano kati ya vijana; Sababu anazozitoa Mzee Isa za kumkatalia salum kutomwoa Rukia hazifai. Mzee anakwepa ukweli wa mambo. Hii ndiyo hali inayopatikana katika jamii nyingi ambapo mwanamume hataki kuonekana kuwa mkosaji.

Angewaeleza ukweli badala ya kutumia vitisho na nguvu ili kunyamazisha uhusiano wao. Hali ya kutokubaliana inajitokeza Rukia anapoendelea na uhusiano wao licha ya upinzani wa babake. Ingawa hawakuoana na Salum ukweli wa mambo unadhihirika
kuwa mkosaji ni mwanamume. Hisia za Rukia zinaeleza hali halisi ya mwanamke aliyegandamizwa na mwenye juhudi za kutaka kujikomboa.

Kitendo chake kinaonyesha jinsi ambayo vijana wanalazimika kupambana katika kukabiliana na kwao na jadi. Tamthilia ya Heshima yangu inashauri waziwazi kwamba katika swala la ndoa, wazee wanapaswa kuwa washauri tu. Mzee Isa anakataa kwa sababu Salum hana wazazi, lakini ukweli ni kwamba yeye ndiye baba wa Salum na Rukia. Endapo wangefunga ndoa basi heshima yake ingevunjika, kwani ndoa kati ya watu wanao husiana kidamu haikuruhusiwa katika jamii za kiafrika.

3:2:2 **TAA SUBI YA KIUME**

Katika tamthilia hii tunaona kuwa kuna kuhiniwa kwa mwanamke na mwanamume katika mfumo wa kijamii na kiuchumi. Tunashuhudia kiburi cha mwanamume cha kujitwaza kwake na kutojali mahusiano na wanawake.

Mzee Isa hajali bibi yake wa halali. anaenda kinyume cha matarajio ya ndoa yao. Anafanya mapenzi na Mama salum na ilhali ana mkewe. Hali hii inadhihirsha kudhulumiwa na kugandamizwa kwa mwanamke katika nyanja ya ngono.

Mama salum anajitokeza kama chombo cha kumfurahisha Isa kwani baadaye anatupwa, hadi tunapoona mzozo kati ya Mzee Isa na Mama Salum kuhusu ndoa ya watoto wao.

Mzee Isa anataka heshima yake ihi fadhiwe kwa kuvunja urafiki kati ya Salum na Rukia na ilhali ndiye aliyewazaa. Mwanamume anaonekana kuwa mwenye kujitakia makuu. Hivyo mwanamke analaumiwa na kupewa jukumu la kumlea mwanaharamu.

EAST AFRICANA COLLECTION

MZEE ISA: Kuomboleza kutafaa nini, mama. Tukae chini tushauriane la kufanya. Umwambie mwanao Salum aache upuzi huu. Walahi heshima yangu. (uk 17)

Mzee Isa anang'ang'ania heshima yake bila kufikiria heshima ya watu wengine. Kunajitokeza hali ya kuonewa ambao hawajali kabisa mambo yanayowakabili wanawake. Ingawa Mama Salum alivumilia kwa muda mrefu ilifikia wakati ambapo hangeendelea kuvumilia.

MZEE ISA: Hawa watoto wetu (anasimama). Loo! Heshima yangu jamani. Heshima yangu ivunjwe katika uzee wangu.

MAMA SALUM: (kwa hasira) kama hutaki kusema lililokuleta hapa toka nyumbani kwangu. Toka nakwambia......(uk 17)

Mama Salum anaona kwamba njia pekee ya kujipatia uhuru wake ni ni kujitenga na mwanamume ili kutofungwa minyororo ya kiitikadi na kijadi inayomnyima mwanamke nafasi ya kushiriki katika juhudi za kuendeleza masilahi yake. Hali hii ndiyo inayosisitizwa na waitifaki wanadhania ya ufeministi asilia kama njia muhimu ya kujikomboa kutokana na udhalimu wa miaka mingi.

Baada ya kugandamizwa kwa zaidi ya miaka ishirini na mitano, Mama Salum anaanza kuona dosari za jamii yake ndipo hataki tena mahusiano yoyote na mwanamume aliye mdhulumu.

Lugano (1989)3 anasema kwamba mfumo wa jamii kongwe umemsaidia mwanamume kujenga fikira kuwa yeye ni bora kuliko mwanamke na kwamba mwanamke ni lazima ajidunishe mbele ya mwanamume. Hii ndiyo hali Mzee Isa aliyotarajia kuiendeleza lakini juhudi zake hazi-kufanikiwa kwani uongo na vitisho vyake vilifikia mwisho baada ya uovu wake kudhihirika wazi. Mwandishi anatuonyasha kwamba heshima aliyoshikilia kwa muda mrefu ilivunjiliwa mbali bila kutarajia.

Mwavita katika Mama Ee baada ya kuvumilia mateso ya mumewe Kinaya kwa muda mrefu, anafikia wakati na kuamua kuishi pekee ili kuepukana na mateso ya mumuwe, ingawa wanawake wenzake wanamwona kama mshindani na mwenye moyo wa kujivuna, anaona kuwa mwanamke ni binadamu kama binadamu yeyote anayeona uchungu ndipo akaamua kuanza kuishi pekee.

Hivyo iwapo wanawake wanataka kufaulu katika vita vyao vya kupigania haki na usawa inafaa wajitie katika rabishe ya kujitetea bila woga.

## 3:3 MWANAMKE KISIASA

Katika tamthilia hii mwanamume anajitokeza kama mwakilishi wa viongozi dhalimu ambao hawajali maslahi ya watawaliwa. Aidha viongozi hawa hutumia mamlaka na vyeo vyao kuwagandamiza wengine Mzee Isa ni kiongozi anayesimamia nyumba kumi kumi kwa sababu hiyo hataki uovu wake ujulikane, hivyo anatumia uwezo wake kamnyanyasa Mama Salum. Uhusiano uliopo katika tamthilia hii kati ya mwanamke na mwanamume ni ule matawala na mtawaliwa. Mwanamke anadhihrika kama mfungwa ambaye hawezi kujitanzua kutokana na minyororo iliyomfunga au kujipatia uhuru kwa njia ya amani. Lazima atumie nguvu katika kupigania uhuru wake.

Lanina katika **Kilio cha Haki 4** anajitokeza kama kingozi wa wafanyakazi ambaye anapigania haki za wanyonge na kupata misukosuko kutokana na msimamo wake madhubuti. anajitokeza kama mtu jasiri na shupavu.

Mama Salum baada ya kudhulumiwa na kunyanyaswa anaamua kumweleza bila kuficha jinsi alivyosumbuka kuubeba mzigo wa aibu wa kuwa na mtoto asiye na baba.

Jambo hili linatudhihirishia wazi juhudi zake za kupinga dhuluma za muda mrefu. Inambidi Mzee Isa kuamua kushirikiana na Mama Salum katika kupata suluhisho la ndoa iliyokuwa imepangwa na watoto wao. Ingawa Mama Salum alikataa kushirikiana naye baadaye tunaona kwamba anatoboa siri ambayo Isa hakutaka ijulikane na jambo hili lina tudhihirishia wazi kuowa mwanamke huyu (Mama salum) ameenda kinyume cha matarajio ya Isa ili kututhibishia uovu aliotendewa, hivyo kuvunja kile kiburi cha Mzee Isa.

## TANBIHI


1. Kitsao J (1980) Uasi Oxford University Press Nairobi

2. Amana B. (1985) Zabibu Chungu Oxford University Press Nairobi

3. Lugano B. (1989) "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi" Tasnifu ya M. A> Chuo kikuu cha Nairobi

4. Mazrui A (1981) Kilio cha Haki Longman Kenay Ltd. Nairobi

# SURA YA NNE

## 4:0 NGUZO MAMA

## 4:1 U TANGULIZI

Tamthilia ya Nguzo Mama inaangazia matatizo yanayowakumba akina mama katika juhudi zao za kujiendeleza. Inaendeleza kwa kinaganaga juhudi zilizofanywa kuwakomboa wanawake kutokana na ukandamizwaji na udhalilishwaji wao.

Muhando ametafakari na kudondoa mikakati ya kuinua hali ya akina mama na nafasi yao katika jamii. Ametumia wanawake tisa ili kuelezea mwamko wa wanawake hao wanaojishughulisha na kazi mbali mbali za kuinua hali zao za kijamii ki uchumi na kisiasa.

## 4:2 U TAMADUNI

Katika tamthilia hii Muhando amewachora wahusika na kike wanaowakilisha jamii ya kiafrika ya jadi ambapo mwanamke anadhihirika kama mtumishi na mwanamume kama bwana.

Engels (1950:9)1 akielezea kuhusu historia ya kugandamizwa na kuanyanyaswa kwa mwanamke katika jamii anasema kwamba wakati mmoja wanawake na wanaume walikuwa na usawa na uhuru. Baadaye

wanawake walipoteza usawa na uhuru wao wa asili na kulazimishwa katika nafasi ya kuwategemea wanaume. Kuanzia wakati huo mwanamume aliwakilisha nguvu za uchumi. Mwanamume alizitumia nguvu hizo kufanya lolote juu ya mwanamke. Uhusiano huo ulizidi kuimarishwa na kukuzwa na taasisi mbali mbali za kijamii, ndoa ikiwa mojawapo ya taasisi hizo.

### 4:2:1 MAPENZI NA NDOA

Mwandishi katika tamthilia hii anatudhihirishia maisha ya ndoa na jinsi yalivyo na shida hasa kwa upande wa wanawake. Tasisi ya ndoa imebomoka kwa sababu ya ulevi na uzinzi.

Wanaume Wamejitokeza kama watu wanaowategemea wanawake kuwapatia chakula hata ingawa hawasaidii chochote. Bwana sudi ni mfano mzuri wa wanaume wanaojishughulisha na mtindi huku mkewe (Bi. Pili) anajishughulisha katika kutekeleza majukumu yote ya familia yao. Bwana sudi anajitokeza kuwa mpinzani wa juhudi za kuendeza ukombozi wa mwanamke kwa kila njia. Anamtisha mkewe kwa kumpiga ili ampe pesa za kuendelea kunywa pombe yake. Hataki na hajishughulishi kwa jambo lolote la maana la kuweza kuleta faida katika familia yake ila kutindi.

Sudi anaamini kwamba nafasi ya mwanamke ni mnyumbani hivyo ni lazima mwanamke atekeleze majukumu yote ya nyumbani kama kuwaliza watoto, kuvua nguo na kulima shamba.

BI PILI: Nimeifua mchana huu. Asubuhi si nili amkia shambani. Kurudi shamba kwanza nikapikia watoto, maji hakuna nikaenda kuyachukua.

SUDI: Kelele sasa mimi nitavaa nini utaikausha kwa moto hiyo nakwambia. Mimi nataka kurudi nilikotoka nimeacha pombe kafiri. Unataka wenzangu waimalize? kausha hiyo nguo kabla sija kupiga...

Bi pili anajishughulisha katika kutekeleza majukumu yote ya familia yao. Ingawa maisha hayo yalikuwa machungu kwake alidhamiria kupata uwezo (wa kuweza) kutekeleza yote yaliyomhitaji. Badala ya kupinga dhuluma kama hii tunaona kwamba Bi pili anakubali unyanyasaji huo.

Baada ya ndoa watu wanapaswa kulinda heshima yao kwa kutoingilia uasherati ili ndoa yao isibomoke. Bi Tano analalamikia hali ya mumewe kwa sababu anajihusisha na uasherati. Watoto wake hawana chakula na

nguo ilhali mume wake Magange anavunja mali na wanawake wengine.

Hali hii ni sawa na ya Mwavita katika Mama Ee (1987)2 ambapo Kinaya hajali wala kushughulika na jamii yake. Amejiingiza katika mtindi na uasherati na arudipo nyumbani anaanza kumpiga mkewe.

Muhando amemchora mwanamke katika mazingira finyu na yenye uonevu. Faida ya kazi yake zinamnufaisha mwanamume. Licha ya matatizo hayo yote hatuoni juhudi za Bi pili na Bi Tano kupinga hali zao dhaifu.

Dahl (1982)3 anaeleza kuwa mwanamke anafaunzwa na kukuzwa akijua kwamba jukumu lake ni jikoni ambapo anahitajika kutunza nyumba, watoto na mumewe. Licha ya hayo yote wanawake huwa wanafahamu njia za kujikomboa kutokana na hali zao dhaifu. Bi pili anaanzisha biashara ili kuchumia wanawe. Biashara hii inamletea faida kubwa ingawa mume anamfilisi. Pia anamuunga Bi Nane kuhusu maoni ya kutumia kamba ambayo inaashiria ushirikiano katika kupigania haki zao. Zaidi ya hayo hakusita kuhudhuria mikutano ya kina mama na kushirikiana nao katika kila hali ya kuendeleza masilahi yao.

Aidha Bi tano amegandamizwa hali kuchukulia hadi yake kama majaliwa. Hajui jinsi ataondoka na shida zilizomzunguka.

Desturi na mila za jadi zinashikilia kwamba milki yote ni ya mwanamume. Na katika desturi za mirathi mwanamke hapewi haki anayostahili kwani anapotalikiwa au anayostahili kwani anapokufa anapokonywa mali yote iliyoachwa na bwanake. Haya ni maonevu yanayo fanyiwa wanawake na jamii ambazo zimetawaliwa na wanaume.

Bi Saba ni mfano mzuri wa mwanamke anayejitahidi kujirimbi kizia mali ambayo ingeweza kumsaidia na jamii yake. Lakini baada ya kifo cha mumewe ananyanganywa mali yote na jamii ya mume wake. Haya yanajitokeza na malalamiko yake (uk 43) ambapo tunadhihirishiwa kwamba jamii ya mumewe walichukua sufuria, kitanda na watoto wake. Kisha wanamzingizia kwamba alikuwa amechukua fedha za mumewe na hivyo walizihitaji. Hali hii inatufanya kutoa madai kwamba jamii ya mumewe wana sheria fulani za kikabila za kurithi mali ya ndugu yao.

Muhando anapotuchorea picha na hali kama hii anataka tufahamu hali halisi ya jamii yake na uovu wanaotendewa wanawake. Hali ya kupora mali ya mjane na baadaye kumfukuza ni dhihirisho la unyama uliokitili mipaka na njia moja ya kumfanya mwanamke kuonekana kama mtumwa anayehudumia tajiri wake.

Haya ni manyanyaso ya hali ya juu anayofanyiwa mwanamke. Hivyo Muhando anajitokeza kushtumu jamii yake kwa kutothamini juhudi za wanawake. Kulingana na nadharia ya ufeministi asilia urithi haupaswi kuegemezwa katika jinsia kama kwamba wanawake si wanadamu.

Ili kujikomboa kutokana na hali kama hii mwandishi anapendekeza kupitia kwa Bi Nane kwamba ni heri wajiunge katika chama cha wanawake ili kupigania haki zao za kiuchumi na kunyonywa na wanaume. Naye Bi pili anajishirikisha katika shughuli za kuendeleza uchumi na hali za kina mama kwa jumla, licha ya juhudi zake za kulima ili kuwalisha watoto wake ilhali mumewe hana lingine la kusaidia jamii yake ila kulewa tu. Bidii zake zina mfanya aanzishe biashara ya kupika pombe. Ingawa biashara hii inachukuliwa kama kikwazo cha maendeleo, pia ni njia moja ya mtu kujipatia pesa.

Anapika na kuuza pombe ili kuchumia wanawe. Biashara hii inastawi na kumletea pesa nyingi ingawa mumewe anamfilisi kwa kunywa pombe yake bila malipo. Juhudi za mwanamke huyu zinadhi hirisha harakati mbali mbali zina zofanya na akina mama katika kujiendeleza. Na mumewe Sudi anawakilisha kundi la wanaume wanaopinga juhudi za wanawake kutokana na taasubi zao. Hakuna uhusiano na ushirikiano baina ya mume na mke ambao ni kipengele muhimu katika ukombozi wa mwanamke.

Mwanamume anawakilisha mawazo ya jamii kongwe ambapo mume ni bwana na mke ni mtumishi na hivyo kikwazo kikubwa cha kumwendeleza mwanamke.

Ingawa Bi Pili anakumbwa na matatizo hayo yote anajitolea mhanga kuendeleza juhudi za kuendeleza hali za kina mama. Anamuunga mkono Bi Nane kuhusu maoni ya kutumia kamba na kushirikiana kwa pamoja katika kupigania haki zao. Vile vile hicha ya kupigwa na kukatazwa na mume kuhudhuria mikutano ya akina mama, hakusita kuhudhuria na kushirikiana na wanawake wengine.

Aidha kuto shirikishwa kwa wanawake katika uchumi kunawafanya kuingilia umalaya. Wanaona kwamba njia pekee ya kujipatia riziki yao ni kuwategemea wanaume. Hali hii ndiyo inayoendeleza kugandamizwa, kudunishwa na kuonewa katika jamii.

Bi Sita analalamika kuwa anahitaji muda ili kuweza kuwanasa wanaume wengi watukaoweza kumpatia pesa. Kuna ukosefu wa mali na kwa hivyo analazimika kushiriki katika uasherati kwa sababu hana njia nyingine ya kujitafutia mtaji. Licha ya hayo bei za bidhaa zina zidi kupanda hivyo kuwa juu na kuathiri uchumi wao.

Ingawa wameathiriwa na uchumi ubinafsi wa wanawake ndio unaojitokeza kama kikwazo cha kuendeleza juhudi zao. Hali ya Bi Sita kumfuata mume wa mwenzake unashusha ubishi badala ya kuungana katika juhudi zao za kujikomboa.

Dosari iliyopo katika vita vyakujikumboa ni ile ya mwanamke kutotilia maanani mbiunu za kumkomboa. Mwanamke anatambua kuwa amegandamizwa lakini bado anaendelea kumnyenyekea mwanamume. Mfano, Bi sita hajishughulishi kujikuza kiuchumi. Anatosheka na hali iliyoko na kuendelea kumtegemea mwanamume. Bi Sita hajishughulishi kujikuza kiuchumi. Anatosheka na hali iliyoko na kuendelea kumtegemea mwanamume.

Bi Tatu naye anakubaliana na mfumo unaomgandamiza. Anamwaona mwanamume kama mtu anayaeweza kumtimizia mahitiaji yake yote, hivyo anajipendekeza kwa mwanamume - Hata anatoroka kutoka shughuli za kuinua hali za kina mama eti kwa kutaka kumpendeza mumewe.

BI TATU: Siyo utani ndugu yangu. Tunakwenda kwenye pati na mume wangu leo saa moja. Lazima nipalilie unga kwa baba watoto wangu eti. Nitakula nini (uk 41).

Huku ni kujinyenyekea kwa hali ya juu hivyo tatizo kubwa katika kuendeleza juhudi za kupigania ukombozi wa wanawake. Aidha wanawake wamegandamizwa hadi kuchukulia hali yao kama majaliwa. Hata hivyo hatua inayohitajika ni kuleta mapinduzi. Mwandishi anadhihirisha kuwa ni lazima kwa kundi la wanawake wanaonyonywa na kunyanyaswa kugundua adui zao na pili kuwa na umoja ili kuleta mabadiliko katika jamii.

## 4.4 MWANAMKE KISIASA

Kutokana na kutokuwepo kwa uhusiano ulio sawa katika jamii mwanamke siku zote ameonekana kuwa mtu ambaye hawezi kuwa na maamuzi yake mwenyewe ila katika matukio fulani fulani. Hii ni dunia ya wanaume. Uhusiano huu usio sawa umewafanya baadhi ya wanawake kujitia katika mstari wa mbele ili kutetea masilahi yao.

Tamthilia hii inadhihirisha mwanamke wa wanawake kisiasa. Baadhi yao wanapigania usawa kisiasa. Baadhi yao wanapigana usawa kielimu, kiuchumi na kijamii kutokana na kukomaa kwao kifikira.

Wanaona kuwa suluhisho la shida za mwanamke katika jamii ni kupata elimu itakayomwezesha kujitambua na kuelewa haki yake. Mawazo ya Bi Nane ni tofauti na ya wengine. Anajitokeza namawazo ya msingi ya

kutaka kuwepo kwa vitendo katika kuinua hali na hadhi ya mwanamke. Anatoa maoni ya kutumia kamba ambazo kwa kweli zikifungwa na kuvutwa inavyohitajika juhudi zao zitafanikiwa. Kamba katika muktadha huu ni taashira ya umoja na ushirikiano kati ya wanaogandamizwa (wanawake).

Mwandishi anamuumba Bi Nane na mawazo yaliyo tofauti na wenzake ili kutuonyesha tofauti iliyopo baina ya wenye elimu na wasiokuwa nayo. Elimu ya kisasa aliyoipata Bi wane inamfanya kuonekana kuwa mwenye uzindushi wa hali ya juu kuliko wengine.

Ingawa elimu yake inasababisha kutoelewana na Bi Nne, ukweli ni kwamba inasaidia katika kuwa zindua wengine ili kuweza kuendeleza juhudi za akina mama.

> BI NANE: Basi tusikilizane. Mnajua nguzo Mama haiwezi kusimama mpaka tuivute kwa kamba. Hebu njooni mchukue hizi kamba tuzifunge
> kwenye nguzo Mama halafu kila mmoja avute.

Anapendekeza matumizi ya naarifa katika kufanikisha juhudi na karakati za ukombozi. Pia anapendekeza kushirikisha watu wangine kama vile watoto na wanaume kwa kuwa maendeleo ya wanawake ni ya watu wote katika jamii.

Licha ya mawazo haya hauwapendeza wengine na kuwavuta, inaonekana kwamba kuna baadhi yao amao hawakuridhishwa nayo, hivyo kudidimiza juhudi za kujiendeleza.

Bi Nne na Bi moja wanapinga mawazo yake (Bi Nane).

Pia swala la uongozi linajitokeza kama kikwazo cha kuendeleza mwamko wa wanawake dhidi ya asasi zina zomdhulumu na kumnyanyasa kwa kila hali. Bi Nne anaongoswa na saikolojia finyu ya kama kuwa kwa kawa yeye ni kiongozi basi anauweza kufanya lolote na watu wamwogope. Anamshtaki Bi Nane lakini alipofikishwa mahakamani hakutamka chochote dhidi ya mashtaka aliyowekewa kwa sababu alifahamu kuwa kungekuwa na hali ya kutoelewana na hivyo kuathiri umoja wa wanawake. Anajitokeza kuwa mwenye busara na hekima.

BI NANE: Nasema na mwenye kiti. Na mwenye kiti uilinde haki yangu ya kuzungumza. Ingawa mimi si kiongozi najua kuwa haki ya kuzungumza ninayo. Siupokei ushauri wako mpaka kwanza nielezwe shtaka lenyewe ni nini hasa. Maelezo yaliyotolewa hapa hayataja shtaka lenyewe nikalielewa.

Bi Nane anaongozwa na elimu aliyonayo katika kufanya mambo. Maazimio waliofikia baada ya mikutano yao mbali mbali ni dhihirisho wazi la mwamko wa wanamwake. Kwa mfano malezi ya watoto kuanzishwa, kuwapa madaraka wanawake, kubadilisha sheria za ndoa na kupinga hali ya watoto wa shule kupewa mimba ovyo. Haya ni baadhi ya matatizo yaliyokuwepo katika jamii lakini.

Wanawake walipaswa kufikiriwa kuwa viumbe vilivyo na usawa na haki hivyo jamii inastahili kujali masilahi yao.
Mwandishi anatudhihirishia kwamba wakati umewadia wa mwanamke kuweza kujikomboa. Anasisisitiza kwamba inawabidi wanawake kuwa na ari yakupinga dhuluma wanayofanyiwa. Anaona kuwa hatua muhimu katika kuleta mapinduzi ya aina yoyote ile, kundi linalodhulumiwa ni lazima litambue kuwa linafanyiwa hivyo na pili kuwa na umoja.

Kile tunachoshuhudia katika tamthilia hii ni kwamba kila mtu anashughulikia mahitaji yake ya kibinafsi hivyo kudidimiza juhudi za kuleta mapambano halisi, badala ya kupigania mambo ya kuwadunisha hususana yale ya jikoni, kulea watoto na kupamba nyumba.

Swala la wivu na ukosefu wa ushirikiano unaathiri juhudi za kujikomboa. Bi Nane ndiye pekee anadhihirika kuwa mpinzani wa dhuluma. Baada ya wengine kutoka anabaki akivuta nguzo Mama.

Mwamko wake unatudhihirishia kwamba wanawake wakitia amri na kupewa nafasi inayostahili watuweza kujitanzua kutokana na minyororo inayowakandamiza.

Lanina katika Kilio Cha Haki 4 anaamua kumkabili adui wake Delamon na kumweleza ana kwa ana matakwa ya jamii iliyonyanyaswa. Ana hamu ya kuipata haki yake ya kujikimu na kujitawala.

Mapambano bi Nane katika tamthilia hii ya Nguzo Mama. Ingawa anakumbwa na matatizo mengi anvyoza katika jiti wanawake ukombozi na anaamini kwamba wanawake watashinda katika mapigano hayo iwepo watakuwa na umoja.

Freire P. (1972) Anasema kwamba: uhuru hupatikana kwa kujipiganiwa wala sio kwa hidaya. Anaendelea kusema kuwa hakuna awezaye kuuelewa umuhimu wa ukombozi isipokuwa yule anayetawaliwa. hivyo ukombozi hauna budi utokane na hao walionynyaswa.
(Tafsiri ni yetu)

Hali hii inatuonyesha kwamab wanaonyanyaswa lazima wawe na mwamko na kufahamu kuwa wameonewa na baadaye waweze kuzua mbinu za kujikomboa. hayo ndiyo malengo ya bi Nane.

**TANBIHI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Engels and Marx | (1950) | Women and Communism. Lawrence and Wilshart london Uk.9 |
| 2 | Mwachofi AS. K. | (1987) | Mama Ee. Heirman Kenya Ltd. Nairobi |
| 3. | Dahl | (1982) | |
| 4. | Mazrui A | (1981) | Kilio Cha Haki Oxford university Press Nairobi |
| 5. | Freire P. | (1972) | The pedagogy of the oppressed. Penguin Books Ltd. middlesex |

# SURA YA TANO

## 5.0 LINA UBANI

### 5:1 UTANGULIZI

Tamthilia hii inajadili matatizo yaliyoikumbwa nchi ya Tanzania baada ya vita vya kagera. Tasnifu hii inadhamiria kuchuguza jinsi matatizo hayo na kudhihirisha jinsi yalivyowaathiri wanawake na juhudi walizofanya katika kujitanzua kutokana na matatizo hayo.

### 5.2 MWANAMKE KIUTAMADUNI

Suala la utamaduni linaambatana sana na nafasi ya mwanamke katika jamii. Hasa tunaporejelea asasi ya ndoa tunaona kwamba asasi hii inamfunga mwanamke na kuathiri maendeleo yake.

Katika tamthilia hii kuna baadhi ya wahusika wanaoshikilia ujadi, kwa mfano mhusika Bibi anapinga ndoa zinazohusisha makabila mbal mbali. Maoni yake ni kuwa kijana wao ni lazima aoe kutoka kabila lao. Uhafidhina kama huu umekuwa kikwazo kikubwa katika kufanikisha harakati za ukombozi.

> Bibi: Baba yako nilimwambia mie kuoa wanawake wa makabila sitaki. Hakusikia. Nilimwambia mie wachusa si watu. (uk 28)

Linalojitokeza ni kwamba Bibi ana sababu zake za kupinga ndoa kati ya Huila na Sara nayo ni chuki inayotokana na ukatili aliofanyiwa mtoto wakewa kike aliyeolewa na Mchusa. Alipata mateso mengi kutoka kwa aila ya mumewe.

Licha ya chuki ya Bibi kwa Sara, hatumwoni Sara naye Kumchukia bali anampenda na kumtunza kama mavyaa. Ametambua kwamba kizazi cha zamani hakiwezi kutambua mabadiliko yanayoikumba jamii ya sasa. Hivyo Sara anawakilisha kizazi kipya chenye mtazamo mpya.

Muhando anajtokeza kuhalalisha ndoa kati ya makabila ili kuendeleza umoja wa wanawake. Anaona kwamba umoja wa Makabila una nafasi kubwa ya kuwaunganisha wanawake. kwa maoni yake ikiwa misingi inayowafunga watu katika makabila hayo tu bali hata kwa wanawake ambao kwa muda mrefu wamegawanyika katika makundi.

Kama tulivyotaja katika tamthilia zake za kwanza, ukosefu wa umoja kati ya wanawake umekuwa kikwazo kikubwa katika kuendeleza juhudi za wanawake za kupigania haki zao. Hata hivyo mwandishi kwa kiwango fulani anadhihirisha kwamba suluhisho la shida za wanawake litapatikana tu iwapo wataungana kama kundi moja lililogandamizwa ili kupigania haki zao.

Kwa sababu ya elimu aliyokuwa nayo, Sara anamhudumia Mvryaa kwa njia ifaayo ingawa kuna ukosefu wa bidhaa muhimu. Kwa upande wa Bibi, ndoa za kikabila zinaathiri umoja wa wanawake katika jamii. Kupigania haki zao, ingawa ana mzinduko, chuki yake kwa Sara inadhihirisha hali yake ya kutokuwa na msimamo kamili kuhusu swala la ndoa. Aidha kifo chake ni dhihirisho la kifo cha kizazi chake kisichoelewa wala kukubali mabadiliko.

Kitendo cha Sara kumfanyia mavyaa wake ilivyo inaonyesha ufahamu wake na anapinga shtuma na vikwazo vinavyozuia muungano wa wanawake. Hivyo anawakilisha kizazi kipya chenye mtazamo na ufahamu wa hali ya juu.

MWANAMKE KIUCHUMI

Katika tamthilia hii tunadhihirishiwa kuzorota kwa uchumi kutokana na vita vya Kagera. Ni jambo lililowazi kwamba vita vinapotokea shughuli muhimu haziendelei kwani hakuna usalama. Vile vile wenye nguvu za kuzalisha mali huingia vitani ili kupigana na adui.

MTAMBAJI: Vita vya Dyamini havikwisha kwani kwisha kwa vita ulikuwa mwanzo wa vilio. Chakula! Hakuna Dyamini mawinguni kashika mvua. Nguo! Hakuna. Wakulima walikwenda vitani pamba hawakulima. Pesa! Hakuna kaiba Dyamini. (uk. 34)

Dondoo hili linatuonyesha hali ilivyokuwa nchini Tanzania wakati wa vita. Uchumi ulizorota na kuathiri wananchi. Licha ya vita, viongozi walianza kuhodhi bidhaa muhimu ili kuwagawia viongozi fulani fulani katika nchi huku wananchi wengine wakiteseka. Walioumia sana ni wanawake kwa sababu jamii nyingi hasa za kiafrika zinachukulia kwamba nafasi ya mwamamke ni jikoni. Hivyo ndiye aastahili kuona kwamba kuna chakula cha kutosha kwa familia yake. Ingawa Huila anafahamu kwamba kuna ukosefu wa chakula na bidhaa muhimu, bado anatarajia kwamba mkewe angetafuta ili kukimu mahitaji ya mamake.

Inambidi Sara kupigana na udhalimu wa viongozi ambao kwa sababu ya uzembe wanapora mali ya umma. Sara ananyimwa bidhaa eti zinapelekwa mitaani na ilhali zina pelekewa wakubwa.

| | |
|---|---|
| SARA: | Nimesema siondoki hapa mpaka nipate mchele, sukari, unga wa ngano na sabuni. |
| SAUTI: | Basi kaa hapo mpaka utakapochoka. |
| SARA: | Ndiyo nitakaa hapa mpaka mtakaponipa chakula. Msiponipa leo kesho nitakaa, na kesho kutua. Nikiondoka bure nitaondoka na mtu. (uk. 37-38) |

Mwanamke katika tamthilia hii amezidukana na anajua hali yake na chanzo cha hali yenyewe. Anafahamu kwamba ananyanyaswa na jamii yake. hali hii ndiyo inayomfanya Sara kujitia katika msitari wa mbele wa kupiga vita hali ya ufisadi.
Anagombana na sauti ambayo inawakilisha viongozi ambao wanaendeleza uovu na uozo wa jamii. Anaukabili uozo huo bila woga. katika hali kama hii mwanamke anaonekana kuwa mwenye uzindushi wa kupigana vita vya uhuru dhidi ya dhuluma za mifumo ya kiuchumi.

Sara ana ujasiri wa kupigania haki yake. Jambo hili lina endeleza mawazo ya nadharia ya ufeministi asilia inayoshikilia kwamba udhalimu wowote unaoendelezwa na jamii ya wanaume ni lazima upingwe. Hivyo Sara anaitisha chakula bila woga na kwa njia hiyo kudhihirisha ujasiri alionao wa kupinga dhuluma.

## 5.4 MWANAMKE KISIASA

Kamusi ya kiswahili Sanifu(1981:259) inaeleza kwamba siasa ni:

> Itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ina msingi wa kuendesha uchumi wake, mwenendo mzima wa maisha ya jamii yako.

Mfumo wa mawazo yaongozayo utawala wa serikali ya Tanzania ni ule wa ujamaa. Serikali ya TANU chini ya uongozi wa mwalimu Juliusi Nyerere ilijiwekea malengo kadhaa ya kujenga ujamaa.

Nyerere (1976:57)2 anaeleza baadhi ya malengo hayo kama; kutoa nafasi sawa kwa watu wote bila kujali rangi uana wala dini, kuondoa unyonyaji, ubaguzi rushwa na ufisadi. Zaidi ya hayo, watu walihitajika kujiunga katika vijiji vya ujamaa bila kulazimishwa na kuhimizwa kukuza mima ambayo ingewaletea faida. Jukumu la serikali na viongozi lilikuwa ni kuwasawishi wananchi ili kuendeleza maendeleo.

Madhumuni ya siasa ya ujamaa ni kujenga jamii yenye haki na usawa. Hayo ndiyo yaliyokuwa matarajio ya wananchi, lakini tunadhihirishiwa kwamba mfumo huu haukuwa tofauti na mifumo mingine iliyopita.

Muhando kwa kumtumia mhusika Bibi anatudhihirishia wazi mifumo iliyopita, na udhaifu wao. Bibi alipitia mifumo ya utumwa, ukoloni, uhuru na ujamaa. Kulingana na maoni yake, mifumo hiyo yote ilikuwa na matatizo. Wananchi walikuwa na matumaini katika mfumo wa ujamaa kuwa ungekuwa mwokozi wao.

Kinachojitokeza ni kwamba, ukosefu wa mwelekeo maalum wa mfumo wa ujamaa ulisababisha maafa mengi kwa wanajamii. Serikali ilitumia nguvu ili kutekeleza malengo yake kinyume na sera za ujamaa.

Kutokana na tajriba ya Bibi tunadhihirishwa kwamba uzindushi wake unamfanya kuwa mpinzani mkuu wa mfumo huu wa kijamaa. Anapinga vikali hali ya kuwalazimisha wakulima kupanda mimea na baadaye kuachwa hadi ikaharibikwa. Kwa mfano serikali iliwalazimisha wakulima kupanda pamba lakini haikuchukuliwa viwandani.
Ili haribikia majumbani mwa wakulima eti kwa sababu ya kuharibika kwa daraja.

Jambo lingine ni kwamba serikali iliiwalazimisha watu kuhama. Nyumba ya Mama senga ilibomolewa na kwa hivyo kulazimishwa kuhamia kwingineko. Mighairi ya hayo, serikali ilijiingiza katika vita visivyofaa bila kufikiria matokeo ya vita hivyo .
Bibi anachukizwa na kifo cha Daudi ambapo Watanzania wanaamua

kuwasaidia waganda kumng'oa Idi Amin mamlakani. Ni kutokana na mwamko wa bibi wa kisiasa ambapo tunamwona akijitia katika harakati za kupinga serikali na mfumo wa ujamaa kwa jumla.

Kwa maoni yetu, Bibi ana ujasiri unaotokana na mwamko au uzindushi aliokuwa nao na kutoogopa. Anaeleza hila za serikali ya Tanzania chini ya mfumo wa ujamaa kwa ujasiri.

Muhando anadhihirika kama mwandishi anayepinga uovu wa viongozi. Kutokana na nyimbo na maombolezo ya bibi, tunagundua kwamba anawasilisha ujumbe wa kuzindua. Anawapiga vita walioko mamlakani, hasa anawashtumu wale wanaopandishwa vyeo na ilhali hawastahili vyeo hivyo.

Zoeni hana elimu lakini ana, cheo kikubwa kushinda wenye elimu. Hali hii inamfanya Bibi kutamba hadithi yake mchana kama njia moja ya kutudhirisha uovu wa viongozi.
Kwa kutumia mbinu ya hadithi mwandishi anatusawiria hali halisi ya jamii yake.

Hata Bwana kata anapandishwa cheo ingawa hakusoma. (uk 12). Ufisadi wa viongozi unawafanya kushikilia matakwa ya wakubwa wao bila kujali kuzingatia matakwa ya wananchi.

Bibi kama mwakilishi wa wanawake na wanyonge kwa jumla anadhihirika kuwa na mzinduko wa hali ya juu. Amezindukana na anashiriki kikamilifu katika mapambano ya kutaka kubadilisha mfumo wa jamii yake. Mwamko wake wa kisiasa unamfanya kukabiliana na nguvu ambazo zinajaribu kumdunisha na kuwaonea raia kwa kupinga matamizi mabaya ya vyeo.

Jamii anayoishughulikia Muhando haionekani kubadilisha msimamo wake kubwa wanawake nasiasia ingawa wanaonyesha uwezo mkubwa. Siasa ya Ujamaa nchini Tanzania ililenga kuleta usawa kati ya watu wake. Lakini hali inayodhihirika katika tamthilia hii ni tofauti. Haionekani kama kwamba kuna usawa wowote. hata hivyo kuna matumaini katika siku zijazo tunapozingatia maneno ya Mota.

## 5.5 MWANAMKE KIELIMU

Mtu anaweza kuelimishwa katika shule, na jamii au tajriba mbali mbali, katika tamthilia hii tunatambua kwamba Mota aliweza kujifunza mengi kuhusu jamii yake na uoza uliokuwepo. Anapata mafunzo muhimu kutoka kwa Bibi ambayo yalimsaidia kuandika ngonjera.

MOTA: Nawambia ndugu zangu hata leo Madyamini wapo. Hapa shuleni kama yule fulani anakaa deski la mbele.

Kuchukua machungwa ya wenzake, Tena
kwa nguvu au kuwadanganya watazame
pembeni Halafu kuwaibia karanga. (uk 55)

Ngonjera hii aliyotunga mota inapinga ukasuku, unyonyaji na udhalimu wa jamii yake. Mawazo haya aliyapata kutokana na hadithi za Bibi zilizomfumbua macho na kuona maovu ya jamii yake.
Elimu ilimsaidia kung'amua matatizo ya jamii na hivyo kumfanya kuwa mwakilishi wa vijana chipukizi na wenye elimu.

Sita katika Zabibu Chungu 3 anakataa ndoa za kulazimishwa kwa sababu ya elimu aliyokuwa nayo. Elimu ina msaidia kutoa sababu zinazowazanga za baba ba mamake.

Hata ingawa Mota ni mtoto anazungumzia maswala kwa njia pevu. Hii ni kutokana na mzinduko wake wa hali ya juu. Muhando kwa kutochorea Mhusika kama Mota, anatudhihirishia matumaini ya kizazi kipya chenye uzindushi wa kuona kwamba kuna hali ya kunyanyasa na ukusefu wa usawa katika jamii.

Anasisistiza umuhimu wa elimu, ambayo waitifaki wa ufeministi asilia walishikilia kuwa njia muhimu ya kuweza kumkomboa mwanamke. Elimu huchochea hisia za mtu na kumfanya kutenda. Ni kutokana na elimu ya Sara na Mota inayowasaidia kuanza kupigania masilahi yao.

# TANBIHI


1. Tuki (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu Oxford Unversity Press Dar-es-Salaam

2. Nyerere J. K. (1976)

3. Amana B. (1985) Zabibu Chungu Oxford University Press Nairobi

## SURA YA SITA

## HITIMISHO:

Katika sura hii tutajajumuisha kwa muhtasari mambo muhimu yaliyojitikeza katika uhakiki tulioufanya. Tutaonyesha matokeo ya utafiti wetu kwa kuzingatia malengo ya utafiti wenyewe.

Madhumuni ya tasnifu hii yamekuwa ni kudadisi dhana ya mwamko wa wanawake katika tamthilia nne za Penina Muhando. Tamthilia tulizozishughulikia ni Hatia (1972)
Heshima yangu (1974) Nguzo Mama (1982) na Lina Ubani (1984) kwa mujibu wa kazi yetu tumejitokeza na mambo kadhaa.

Kwanza, Muhando anaonekana kuwa mweledi wa matatizo ya wanawake. Kutokana na tajriba aliyonayo anadhihirika kuyazungumzia matatizo yanayowakumba wanawake kwa njia inayofaa.

Kulingana na maoni yake inafaa jamii yo yote ya wanadamu iwe na ari ya kuleta haki na usawa kati ya wanawake na wanaume. Anasisistiza kuwa juhudi za wanawake na wanaume zinahitajka ili kuleta ukombozi wa wanawake.

Muhando anatudokezea wasia kuwa na mwelekeo wa kuweza kumpiga vita mwanamume. Hata hivyo kuna baadhi yao walio na urazini wa hali ya juu.

Anatuchorea jamii zenye matatizo na hali isiyo ya kuridhisha. Jamii ya tamthilia hizi zinamulika hali ya jamii mahsusi ya mwandishi huyu na hali ya jamii nyingine katika Afrika. Jamii ya Hatia inadhihirisha dhuluma ya wanawake katika nyanja mbali mbali za maisha, Uchumi, sheria n.k.

Cheja katika tamthilia hii anawakilisha kundi la wanawake walionyonwa. Tunakubali kuwa ni msichana aliyelelewa kijijini na alipoletwa mjini analimbukia maisha ya mjini.

Licha ya dhuluma alizokumbana nazo, tunamwona akikua na kubadilika kutokana na motisha kadhaa zikiwemo za kisilika na na kimazingira na jinsi zilisvyoathiri maisha na vitendo vyake kwa jumla.

Alikumbana na matatizo na masaibu wanayopitia wanawake wengine. Hata hivyo anafikia uamuzi ambao wanawake wenye mawazo ya kujikomboa wanatarijiwa kuwa nayo.

Ingawa kunajitokeza hali ya udhalimu na udhalilishwaji wa wanawake, mwandishi anatuonyesha kwambaa njia pekee ya kutokana na hali hizo

ni kujitegemea kwa mwanamke katika kila hali. Anatuchorea harakati za wanajamii katika kutatua matatizo yao.

Katika tamthilia ya Heshima Yangu mwandishi anaendeleza swala la dhuluma na unyanyasaji wa wanawake. Rukia na Mama Salum ni mfano mzuri wa wanawake wanaodhumiwa na jamii husika. Hata hivyo Muhando anatuonyesha kukua na kujihamasisha kwa mwanamke kila uchao. Rukia anajibidiisha kudumisha uhusiano wake na Salum licha ya pingamizi za babake. Naye Mama Salum hataki kushirikiana na Mzee Isa katika kuwakanya Rukia na Salum kuendelea na mapenzi yao. Anaamua kueleza uovu wa Mziee Isa kwa walimwengu.

Kutokana na juhudi za wanawake hawa tunaweza kutoa madai kuwa wamepata mwamko mpya. Anatuhimisha kuwa ni lazima tutambue kwamba wanawake nao wanastahili heshima.

Brecht anasisitiza kwamba tamthilia nzuri siyo tu ile inayowakilisha matendo ya binadamu bali ile inayotoa kidokezo kuhusu kiini cha matendo hayo na hali halisi inayoyazaa.

Vile vile tunaamini kwamba fasihi yoyote ile inahitaji kuboresha maisha ya binadamu. Mwanafasihi ana jukumu la kuisawiri jamii kwa uangulivu na umakinivu wa hali ya juu.

Katika tamathilia ya Nguzo Mama Muhando amepiga hatua katika kutafakari na kudondoa mikakati ya kuinua hali ya akina Mama na nafasi yao katika jamii. Hata hivyo anadhihirisha kuwa ukosefu wa umoja ndio unaorudisha nyuma juhudi hizo. Baadhi ya wanawake katika tamthilia hii hawajui adui yao ni nani. Hivyo ukosefu wa mbinu dhabiti za kujikomboa ndio unaodidimiza mwanamke katika unyonge na udhaifu.

Mwandishi anawashauri kwamba inawabidi kabla ya kuingia vitani vya kujikomboa kumwelewa adui yao ni nani kutafuta na kufahamu asili ya ugandamizwaji wao. Kuna matumaini kuwa watapata uokovu kwani wameguswa na mwamko mpya wa kisiasa, kijamii na kiuchumi na mfano mzuri ni Bi Nane.

Lina Ubani ni tamthilia inayosisiti za kwamba wanawake wanahitaji elimu na ujasiri wa kutosha ili kuwawezesha kujikomboa kutokana na dhuluma za wanaume na jamii kwa jumla.

Wanawake katika tamthilia hii wamejitambua kama viumbe walio na haki ya kujiendeleza kama wanaume. Mfano Bibi na Mota wana ujasiri na ndiposa wanajitokeza kuwa wapinzani wa mifumo inayoendeleza dhuluma.

Tumeangalia jinsi mwandishi anavyowasawiri wahusika wa kike na tumeona ku katika vipengele vya jamii uchumi elimu na siasa mwanamke anadhihirika ka kiumbe duni kisichotaminiwa na jamii inayozunmziwa. Mighairi ya hayo, k maendeleo fulani katika wandishi wake hasa jinsi anavyoendeleza maudhu wanawake. Anakuza maudhui hayo kulingana na hadithi zake ziuza. Anadhihir kuwakuna matumaini ya kubadilisha hali na hadhi ya mwanamke katika j ambayo imeenea dhuluma.

## BIBLIOGRAFIA:


| | | |
|---|---|---|
| Adagala K. | (1981) | Wanja of Petals of Blood. A study of the Woman question and imperialism in Kenya staff seminar paper University of Nairobi |
| Adeola J. (ed) | (1990) | In Their Own Voices, African Women writers talk James Currey London. |
| Amana B. | (1985) | Zabibu Chungu, Oxford university Press Nairobi |
| Aristotle | (1988) | The politics Cambridge press |
| Balisidya M. | (1975) | Hatia Makala katika Mulika na 7 Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili Dar-es-Salaam |
| | (1982) | The Image of women in Tanzania Oral literature makala katika Kiswahili Juzuu 49/2 Taasisi ya uchunguzi wa kiswahili dar-es-Salaam |

(1987) Makala katika Kiswahili Jizuu 54/1 and 2 Tuki Da-es-Salaam

Banks O. (1981) Faces of Feminism A study of Feminism as a social Movement, Basil Blackwell

Chacha N.C (1982) Mke Mwenza, Heinman Educational Books Ltd. Nairobi.

(1986) Mazingira ya Mwanamke katika fasihi ya kiswahili Rosa Mistika wa E. Kezilahabi Mwamko Jarida la chama cha kiswahili chuo kikuu cha Nairobi

Dhahabu L. G. (1994) Uumbaji na Uendelezaji wa Wahusika katika tamthilia za Penina Muhando. Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Nairobi

Egner D. (1981) The Gender Benders. A look at the trenders Distorting The Roles of Men and Women, Radio Bible class, Michigan

Engels F. (1950) Origin of the family katika Women and Communism Laurence and Wishart, London.

Forster E.M. (1973) Aspects of the Novel, penguin London

(1971) Wakati Ukuta East african publishing House Nairobi

Hamilton R. (1978) The Liberation of women a study of patriachy and capitalism, George Allen and Unwin publisher Ltd. London.

Holter H. (ed) (1984) Patriarchy in a Welfare society, Universitet foulaget, Oslo

Hussein E. (1969) Kinjeketile, Oxford University Press, Dar-es-Salaam

(1971) Wakati Ukuta, East African publishing House, Nairobi

(1980) Arusi, Oxford University Press Nairobi.

(1988) Kwenye Ukingo Wa Thim Oxford University Press Nairobi

Jaggar A.M. (1983) Feminist Politics and Human Nature. Rowman and Allanheld publishers, New Jersey

Jaquette J.S. (1974) Women in politics, John Willey and sons, Newyork

Kate, Carol, Rosely (ed)(1988) Of Marriage and the (Marxist). Women's surbodination Internationally and its lesson. Routledge and Kegan, London

Kamunde M.E. (1983) Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Nairobi

Kamusi ya kiswahili sanifu(1981) Oxford University Press, Dar-es-salaam

Kiango S.O (1992) Taswira ya mwanamke katika Tamthilia za kenya.
Makala katika Baragumu Jarida la chuo kikuu kishirikishi. Maseno

Kitsao J. (1980) Uasi Oxford University Press Nairobi

Lugano R.S (1989) Mwanamke katika Riwaya za kezilahabi Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Nairobi

Marzui A. (1981) Kilio cha Haki Longman Kenya Ltd., Nairobi

Mbughuni O. (1982) The image of Women in kiswahili prose fiction makala katika Kiswahili Juzuu 49/1 Tuki Dar-es-Salaam

Mitchel J. (1966) Women The Longest Revolution Essays in feminism literature and psychology Virago Pess Ltd. London

Mochiwa Z.S.M. (1976) Hatia makala katika Mulika nambari 8 Taasisi ya uchungusi wa kiswahili, Dar-es-Salaam

Mugambi P.J. (1982) Uhakiki wa Maadhui katika tamthilia za kikenya zilizochapishwa Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Nairobi

Muhando P. (1972) Hatia East African Publishing House Dar-es-Salaam

(1974) Heshima Yangu East African Publishing House Nairobi

(1982) Nguzo Mama Dar-es-Salaam University Press, Dar-es-Salaam

(1984) Lina Ubani, Dar-es-Salaam University Press, Dar-es-Salaam

Mwachofi A.K. (1987) Mama Ee Heinman Kenya Ltd., Nairobi.

Ndungo M. (1985) Wanawake na Mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya kiswahili tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Nairobi

Nicholson L.J. (1986) Gender and History, Columbia University Press London

Ngugi T. (1981) Writers in politics Heinman Educational Books Ltd. Nairobi

O.E.C.D. (1979) Equal Opportunities for Women Paris

Oskaya G (1981) From captivity to Freedom , A woman's fight. Ankara

Plato (1955) The Republic Penguin Books Ltd. Baltimore

Pock-J-na coyle M. (1984) Literary Terms and Criticism Mackmillan London

Saadawi E. (1980) The Hidden Face of Eve women in Arab World Ltd. Press London

Tutle L. (1986) Encyclopaedia of Feminism, Longman group Ltd. London

Webster (1951) Webster's Collegiate Dictionary London.

Wolstonecraft M. (1985) A Vindication of the Rights of Woman The subjection of women, Rent and sons Ltd. London

Zaja O. The short Distance runners. A case study of the works of Peninah Muhando and Jay kitsao Mwamko volume 3. Jarida la chama cha kiswahili cha chuo kikuu cha Nairobi.